

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA

(Barua zote majibu kwa Mkurugenzi Mtendaji)

SIMU: 0732 932312
FAX: 0732 932359
Email: dedruangwa@gmail.com
Web: www.ruangwadc.go.tz
Blog: www.ruangwa.blogspot.com



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA,
S.L.P 51,
RUANGWA.

Kumb Na. HWR/K.2/15/95

27/03/2018

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kwa mujibu wa kibali cha Ajira Kumb.Na.CFC 26/205/01'FF'/91 cha tarehe 22 Agosti, 2017 kama kilivyoongezewa muda kwa kibali Kumb.Na.CFC.26/205/01"GG"/95 cha tarehe 12 Machi, 2018 kutoka kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa anawatangazia nafasi za kazi Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi:

❖ **MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – (NAFASI 44)**

A: Sifa:

Mwombaji awe amefaulu kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyefaulu mafunzo ya Astashahada/Cheti "NTA Level 5" katika moja ya fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

B: KAZI NA MAJUKUMU YA AFISA MTENDAJI WA KIJIKI

- 1) Kukusanya mapato ya Halmashauri ya Wilaya
- 2) Afisa Masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- 3) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- 4) Kuratibu na Kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- 5) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- 6) Kutafsiri na Kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- 7) Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Kazi katika eneo lake na Kuhamasisha wananchi katika kuandaa na Kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- 8) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalamu katika ngazi ya Kijiji
- 9) Kusimamia kukusanya na Kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Serikali ya Kijiji
- 10) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji

- 11) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata
- 12) Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri

C: Ngazi ya Mshahara

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji daraja la III kina ngazi ya Mshahara TGS B

D: MASHARTI YA JUMLA

- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutumwa kwenye anwani iliyotajwa hapa chini.
- Mwombaji aambatanishe nakala za vyeti vyake vya taaluma, cheti cha kuzaliwa, Maelezo binafsi (CV) na nyaraka zote muhimu pamoja na picha 2 (passport size) zilizopigwa hivi karibuni.
- Testimonials "provisional results" "Statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita **(FORM FOUR AND FORM SIX RESULT SHEETS) HAVITAKUBALIWA.**
- Nafasi ya kazi aliyombwa iandikwe juu ya bahasha, kutozingatia hili kutasababisha maombi ya kazi kuwa batili.
- Kwa wale watakaopita kwenye mchujo wa awali (Short listed candidates) ndio watakaoitwa kufika kwenye usaili (Interview) na kufika na vyeti halisi.
- Barua zote za maombi ziandikwe na kutumwa kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUANGWA,
S.LP 51,
RUANGWA.

NB: Uwasilishaji wa barua za maombi kwa mkono katika ofisi za Halmashauri ya Wilaya hazitapokelewa.

Mwisho wa kutuma na kupokea maombi ni tarehe **09 Aprili, 2018**



ANDREA G CHEZUE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
JISIRI **RUANGWA** DIRECTOR
RUANGWA DISTRICT COUNCIL

Nakala:

- Website ya Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Blog & Radio Ruangwa
- Katibu Tawala (Mkoa)
- Mbao zote za Matangazo Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa
- Wah. Madiwani